# Usaidizi wa Sehemu ya 4

Aprili 2011

Section 4 support - Swahili

## Usaidizi wa Sehemu ya 4 ni nini?

Iwapo dai lako la utafutaji kimbilio litakataliwa kabisa, usaidizi utakaopokea wa kimbilio kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani utakwisha. Utapokea barua kutoka kwa Ofisi hiyo ikikueleza hviyo. Hata hivyo, unaweza kuhitimu kupata usaidizi wa Sehemu ya 4. Usaidizi huu ni wa muda mdogo unaotolewa na Ofisi ya Nyumbani lakni ni tofauti na usaidizi uliokuwa ukipokea hapo awali kwa njia kadhaa:

1. **Kadi ya Azure:** Hutapokea pesa zozote. Usaidizi wako wa kila wiki utakuwa ukiwekwa kwenye kadi ya malpo ya 'Azure'. Kadi hii ya Azure inaweza kutumika katika maduka fulani kama Asda na Tesco ili kununua vitu muhimu kama chakula, vifaa vya mwili, na vya kusafishia.
2. **Makazi ya kushiriki:** Iwapo hujaolewa, utahitajika kushiriki nyumba moja na watu wengine wa jinsia kama yako;
3. **Makaazi yasiyo ya kuchagua:** Utapata nafasi moja tu katika nyumba katika makao ya Sehemu ya 4. Ikiwa utakataa kuichukua, kwa sababu yoyote ile, Ofisi ya Nyumbani inaweza kuondoa usaidizi wako; na
4. **Hakuna chaguo la 'usaidizi-pekee' :** Hakuna chaguo la kufanya mipango yako mwenyewe ya makazi **na** kupokea vocha za malipo ya Sehemu ya 4.

## Ni nani anastahili kupata usaidizi wa Sehemu ya 4?

Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti inaweza kukusaidia kutuma ombi la usaidizi wa Sehemu ya 4 iwapo ko fukara na unafaa chini ya **moja** ya njia zifuatazo:

1. **Dai mpya la utafutaji kimbilio/dai la haki za kibinadamu:** Iwapo mwakilishi wako wa kisheria ametoa dai mpya ya utafutaji kimbilio au rufaa iliyochelewa. Dai hilo litahitaji kuwa limetumwa na tutahitaji nakala ya makaratasi yote uliyotuma;
2. **Ukaguzi wa kimahakama:** Iwapo mwakilishi wako wa kisheria ametuma ukaguzi wa kimahama na Korti la Kikao. Tafadhali tupe na nakala ya makaratasi yote yanayohusika na kesi hii kutoka kwa wakili wako;
3. **Asiyestahili kusafiri:** Iwapo kuna sababu ya kimatibabu ambayo inakuzuia kusafiri kurudi nyumbani. Njia ya hii huwa kali sana. Utastahili iwapo uko zaidi ya miezi 7 ya kuwa mjamzito au iwapo una taarifa iliyoandikwa na daktari akisema "hustahili kusafiri". mengi ya matatizo hayazingatiwi kuwa mazito ya kutosha;


Scottish Refugee Council is a charity registered in Scotland.
Registered Charity: SC008639

4. **Hakuna njia salama:** Ni ngumu sana kufikia kiwango hiki. Kulingana na Ofisi ya Nyumbani, hakuna nchi yoyote kwa sasa ambayo njia hii hutumika. Washauri wetu au mwakilishi wako wa kisheria ataweza kukueleza iwapo hili limebadilika; au

5. **Kurudi kwa Hiari:** Iwapo unaweza kuthibitisha kuwa unachukua hatua za kurudi yako ya asili. (Tazama chini kwa "Kurudi katika nchi yako ya asili?")

**Ushahidi wa ufukara**

Ili kustahilikupata usaidizi wa Sehemu ya 4, lazima uwe bila usaidizi wa aina yoyote ile. Iwapo umesaidiwa na marafiki, jamii au kikundi cha kidini utahitaji kueleza ni kwanini hawawezi kuendelea kukusaidia.

Iwapo hii ni hali yako, tafadhali tuletee barua kutoka kwa watu ambao wamekuwa wakikusaidia, ikionyesha ni nani, jinsi walivyokuwa wakikusaidia, kwa muda gani na ni kwa sababu gani hawawezi kuendelea na kukusaidia. Jambo hili la mwisho ni muhimu sana.

**Ombi hili la Sehemu ya 4 huchukua muda gani?**

Linaweza kuchukua wiki mbili kwa Ofisi ya Nyumbani kutengeneza ombi lako. Tutaangalia mwendo huo mara kwa mara na tutawasiliana nawe punde tutakavyopata uamuzi, kwa hivyo hakikisha kuwa na tondoti zako za kuwasiliana nawe na utueleze iwapo utabadilika. Sio lazima uje ofisini mwetu kutazama jinsi ombi lako linaendelea. Iwapo ungependa, unaweza kutupigia simu kupitia nambari yetu ya bure 0800 085 6087(ya bure kutoka kwa simu za nyaya lakini sio kutok akwa simu ya mkono).

Iwapo utakubalika kupata msaada wa Sehemu ya 4, utapigiwa simu na mkimu wako wa makao ili kupanga tarehe ya kwenda kwa makao unayoishi.

Mwakilishi atakuonyesha makao, na tondoti za kuwasiliana naye na kukuuliza kuia saini makubaliano ya makazi. Mkimu wako wa makazi anawajibika kwa utengenezaji wa makao yako. Iwapo una maswali kuhusu makao yako, wasiliana na mwakilishi wako kwa kutumia tondoti walizokupatia.

**Rufaa**

Iwapo ombi lako limekataliwa, tunaweza kukata rufaa kwa niaba yako. Hili litalingana na sababu ambao Ofisi ya Nyumbani itakupa usaidizi wa kukataa. Ukataji rufaa utapitia kwa shirik ahuru linaloitwa First Tier Tribunal (Usaidizi wa Utafutaji Kimbilio) lililo, Croydon, London. Unaweza kuhudhuria rufaa hiyo iwapo ungependa kutetea kesi yako. Ofisi ya Nyumbani itagharamia safari yako na makao iwapo utawaeleza kuwa ungependa kuhudhuria.

**Unarudi kwa nchi yako ya asili?**

Iwapo ungependa kujua usaidizi wa kurudi kwenye nchi yako ya asili unaweza kuwasiliana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) katika ofisi yao ya Glasgow katika anwani ifuatayo:

**International Office of Migration (IOM)**
38 Queen Street, Glasgow
Kwa miadi piga simu katika: 0141 548 8116

**Mapendekezo na malalamiko**

Mwitikio wako unakaribishwa na utatusaidia kukuza maelezo na huduma zetu.

Iwapo ungependa kutoa pendekezo kuhusu jinsi tunavyoweza kukuza huduma na maelezo yetu, tafadhali kamilisha fomu yetu ya mwitikio. Unaweza kupata fomu kutoka kwa wafanyakazi wetu katika ofisi yetu na uipakue kutoka kwa tovuti yetu:
http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/assets/0000/0183/Complaint_leaflet_English_March_2010.pdf

Tafadhali rudisha fomu iliyokamilishwa kwa ofisi yetu.

Unaweza pia kulalamika kwa Ofisi ya Kamishna wa Uhamiaji (OISC): http://www.oisc.gov.uk/